Réseau des Femmes pour la défense Des Droits et la Paix

R.F.D.P

Téléphone : + 243 (0) 813181854
+ 243 (0) 817984427
+ 243 (0) 997756461

E-mail : rfdp1999@yahoo.fr / Av. Fizi n° 41/05 / Commune d'Ibanda - Bukavu RD Congo

# KUPIGA MARUFUKU UJEHURI KUPITIA VIUNGO VYA UZAZI NA KUAZIBU VIKALI

## KUPIGANISHA UJEHURI KUPITIA VIUNGO VYA UZAZI WA AINA YOYOTE



UJEHURI KUPITIA VIUNGO VYA UZAZI unamaana gani?
Azabu ni gani?

Cordaid

# KUPIGA MARUFUKU UJEHURI KUPITIA VIUNGO VYA UZAZI NA KUAZIBU VIKALI

## KUPIGANISHA UJEHURI KUPITIA VIUNGO VYA UZAZI WA AINA YOYOTE

## UJEHURI KUPITIA VIUNGO VYA UZAZI: unamaana gani? Azabu ni gani ?

*Sheriya namba 06/018 ya tarehe 20 mwezi wa saba mwaka wa elfu mbili na sita (2006) inayo badili na kuongeza agizo (amri) ya tarehe 30 mwezi wa kwanza mwaka elfu moja mya kenda makumi mane (1940) zidi ya buku la hukumu ya jamuhuri ya kidemokrasya ya Congo.*

**Sababu gani Kutangaza sheriya hiyo !**

Tangu nusu karni iliopita kipindi cake ca pili, kumejitokeza hali mbovu ya mauwaji na pia ujambazi kote ulimwenguni. Hali ambayo ilisababishwa na kutafuta faida za kiucumi, kijamii na kisiasa. Mauwaji hayo na hali hio ya ujambazi vilikomalisha ujehuri kupitia viungo vya uzazi.

Vita vya mwaka wa elfu moja mya kenda makumi kenda na sita (1996) na ile ya elfu moja mya kenda makumi kenda na nane (1998) inchini mwetu (DRC)

iliharibu mambo yote. Wakati ule kukajitokeza uhaba wa ucumi na kuweko kwa watu wengi wahanga wa jambo hilo. Wengi wao wakiwa na matatizo ya kila aina. Wahanga wote wale wanaishi katika hali ya kukosewa heshima kiutu pia kimwili. Matendo kama na haya hayawezi baki bila kuazibiwa kwa siku za usoni.

Kuona umuhimu wa kukinga na kuazibu vikali makosa za ubakaji wowote na kuwashurulikiya wahanga wa makosa hayo, ilionekana ni vema kubadili vipengele ama nugta fulani fulani katika kitabu ca hukumu incini jamuhuri ya kidemokrasya ya Congo.

Hadi hapo, sheria ya hukumu ya jamuhuri ya kidemokrasya ya congo haikuwa bado na tuhuma ama jisi zote ambazo sheriya ya kimataifa inataja kuwa makosa kama msingi wa haki toka mwaka wa elfu moja mya kenda makumi mane na sita (1946) kwa wale wadogo kama vile wakubwa, wanao vunja sheria ya kimataifa ya kiutu ili watu wote wa dunia nzima waishi katika hali yenyi samani ya kiutu.

Kwa hiyo, sheria hii nyipia inabadilisha na kuongeza katiba ya hukumu ya jamuhuri ya kidemokrasya ya congo kwa kuongeza taratibu za sheria ya kimataifa ya kiutu kuhusu ujehuri kupitia viungo vya uzazi.

Sheria hii inahusika hasa zaidi na ukingo wa watu wahanga wa ubakaji wakiwemo kati yao wanyonge. Akina mama, watoto na wanaume. Sheriya hii inaleta mcango ili kugeuza niya mbaya katikati ya watu, kurudisha hali bora ya usalama unaodumu incini.

Kulingana na kitabu ca hukumu, mabadiliko hayo yanahusika zaidi na makosa zidi ya ubakaji na ukosefu wa heshima kwa viungo vya mwili. Vipengele vilivyo tayarishwa vinatafautisha makosa zidi ya ujehuri kupitia viungo vya uzazi vya kila namna na kila aina ya makosa ambazo hazikuweko na kuonyeshwa katika buku la hukumu. Pia vipengele hivyo vinatowa mafasirio kamili kuhusu ubakaji kulingana na mwenendo wa sheriya ya kimataifa.

SHERIA

Bunge la taifa limekubali ;
Raisi wa jamuhuri anatangaza sheria ambayo ifwatayo:

**Kipengele ca kwanza:**
Kumeongezwa mkondo (section) wa kumi kwa buku la kwanza la kitabu ca hukumu ambao inasema hivi:

**Mkondo wa Kumi** (Section X) : Kuhusu upungufu wa muhimu, hali fulani ya ceo na taratibu zidi ya ujehuri kupitia viungo vya uzazi.

**Kipengele ca 42 (bis)**
Hali ya mtu kiserkali anayehusika katika kosa zidi ya ujehuri kupitia viungo vya uzazi haiwezi hata kidogo kusababisha asiazibiwe ama kupunguziwa azabu.

**Kipengele ca 42 (ter)**
Kuwa mwenyi ceo ama kuwa na uongozi hata kwa ngazi za juu ki raia ama kijeshi haiwezi sababisha mtu ambaye aliendesha njama za ujehuri kupitia viungo vya uzazi asiazibiwe.

**Kipengele ca pili :**
Mkondo wa pili, kicwa ca VI kwenyi kitabu ca pili ca hukumu ulibadilishwa na kuongezwa kama ifatavyo :

**Mkondo wa pili : kuhusu makosa ya ujehuri kupitia viungo vya uzazi**

**Sura ya 1 : Kukosa heshima kwa viungo vya mwili**

**Kipengele ca 167 :**
Kila kitendo tofauti na tabia za heshima ambazo hufanyika kwa kusudi kwenyi mwili wa mtu bila makubaliyano yoyote ni kukosa heshima kwa mwili wa mtu yule. Ukosefu wa heshima kwa mwili wowote ambayo hutendeka bila ujehuri ama vitisho kwa mtu mzima kwa msaada wa mtoto mwenye kuwa na umri

ya myaka chini ya kumi na minane, utaazibiwa kifungo ca myezi sita hadi myaka mitano gerezani. Umri ya mtoto inapashwa tajwa kiisha ucunguzi wa mganga ingawa hakuna ceti ca serkali ca raia.

**Kipengele ca 168 :**
Kukosa heshima kwa watu haizuru wa kiungo gani ca uzazi katika hali ya ujehuri, ujanja ama pia mashambulizi, hukumu ni kifungo toka myezi sita hadi myaka tano.

Kukosa heshima kwa mtu wala kumutendea kitu kwa mwili wake kwa kinguvu, katika hali ya mazarau ama ujehuri pia vitisho ama kwa kutumia mtoto wa myaka cini ya kumi na minane, azabu ni kifungo ca myaka tano ama kumi na mitano.
Ikiwa kisa hiyo ilifanyika kwa watu ama kwa kutumia watu wenye myaka chini ya kumi, azabu itaenda toka myaka tano hadi makumi mbili (ishirini).

## Sura ya 2 : Kuhusu ubakaji

**Kipengele ca 170 :**
Atafanya ubakaji kwa ujehuri ama kwa kinguvu, ama pia kwa mashambulizi akiwa peke yake wala akitumikisha mtu mwingine wala tena ikiwa ni kwa kumshitukia na kupoteza akili yake, ama kutokana na mazingira mabaya ao kupitiya ugonjwa fulani ama

ulemavu wa mtu pia tukio lolote ama kuwa amepoteza kiungo kimoja kwenyi mwili mpaka kukosa uwezo yoyote.

a) Mwanaume yeyote haizuru wa umri gani, atakaye ingiza (penyeza) kiungo cake ca uzazi yulu yulu ama ndani ya kiungo ca uzazi ca mwanamke ama kila mwanamke haizuru mwenyi umri gani ambaye atamushurtisha mwanaume kuingiza kiungo ca uzazi ndani yake ;

b) Kila mtu atakae ingiza kiungo ca uzazi ama kitu fulani hata kwa juu, ndani ya tundu ya lazima kubwa (anus), ndani ya kinywa ama tundu yoyote inayopatikana kwenyi mwili wa mwanamke ama mwanaume ;

c) Kila mtu atakae ingiza hata kwa juu, kiungo kingine ca mwili ama kitu (combo) kingine ndani ya kiungo ca uzazi ca mwanamke ;

d) Kila mtu atakae shurtisha (lazimisha) mwanaume ama mwanamke kumuingiza hata kwa hali ya juu juu kiungo ca uzazi ama kingine ndani ya tundu ya lazima kubwa, ndani ya kinywa ama kwenye tundu ingine mwilini mwake, kwa hiyo mtu anaye shutumiwa kama mubakaji, atapewa malipizi ya kifungo tangu myaka tano hadi makumi mbili na kulipa kwa serkali kiwango ca pesa elfu mya moja na kuzidia: franka za Congo zinazo linganishwa na pesa za msimamo. Hali hiyo itaitwa ubakaji

kwa kutumiya nguvu hata kama ni kukutanisha tu viungo vya uzazi vya watu ambao wanatajwa kwa kipengele ca 167, aya yake ya pili.

**Kipengele ca 171 :**
Ikiwa ubakaji ama kutokuheshimu kwa mwili unasababisha kifo ca mtu ambaye kutendewa hivyo mutuhumiwa atahukumiwa kifungo ca maisha ndani ya jela.

**Kipengele ca 171 bis**
Azabu ndogo ambazo zinapatikana katika vipengele vya 167 mustari wa pili ;168 na 170 mustari wa pili katika kitabu ca Hukumu hiki zitazidishwa mara pili :

1) Ikiwa washutumiwa ni watu wa jamaa moja na mtu ambaye ni mwenyi kuhafiriwa na vitendo hivi ama mtu ambaye kupitiya kwake vitendo hivi vilifanyika.

2) Ikiwa wanaweza kukamata hatuwa fulani kwa ajili yake yaani wana mamlaka fulani juu yake.

3) ikiwa ni walimu ama wafanya kazi wa watu ambao hutajwa hapa juu ;

4) Ikiwa uhalifu ulifanyika labda na wafanyakazi wa serkali ama viongozi wa kanisa ambao kutumiya vyeo ambavyo wanashikilia kanisani ili kutenda hayo, ama na waganga wakienyeji wasaidizi wa kijamii kwa watu ambao wana halika kupata msada kwao.

5) Ikiwa mushutumiwa alisaidiwa kwa tendo hilo la uhalifu na mtu mumoja ama watu wengi.

6) Ikiwa uhalifu ulifanyika kwa watu ambao hushikiliwa na watu wenye kuwachunga ;

7) Ikiwa ulifanyika hazarani ;

8) Ikiwa ulisababisha kwa muhanga uhaba wa afia na kuacha vinyume kimwili na kififikra

9) Ikiwa ulifanyiziwa mtu anayeishi na ulemavu.

10) Ikiwa ubakaji ulifanyika kwa vitisho vya silaha; Ikiwa hali ya ubakaji kama ilivyotajwa kwa nugta ya 1 na ya 2 kwa kistari ca 1, muamzi ataondowa mamlaka ya uzazi ama ya uchungaji kama inavyo andikwa kwa Kipengele ca 319 ca kitabu ca sheriya ya jamaa.

**Kipengele ca tatu :**
Mkondo wa III kwa buku la VI la kitabu ca II ca hukumu ambayo inabadilishwa hivi :
Mkondo wa III : Uhalifu ungine wa ujehuri kupitia viungo vya uzazi.

**Sura ya 1: kuhusu kusababisha watoto kufanya usharati.**

**Kipengele ca 172 :**
Mtu ambaye atavunja mila kwa kusababisha, ili kumaliza haja ya mwengine, usharati ama ulaji wa rushwa wa watu mbalimbali wa umri wa chini ya myaka kumi na minane atahazibiwa kwa kufungwa gerezani miezi tatu hadi myaka tano na malipo kwa serkali franka tangu elfu makumi tano hadi elfu mya moja za kikongomani zenyi kulinganishwa na pesa za msimamo.

**Kipengele ca 173 :**
Mambo ambayo hutajwa katika kipengele cha juu yatahazibiwa kwa kufungwa gerezani myaka kumi hadi ishirini na kulipa kwa serkali franka za kikongomani elfu mya moja mpaka elfu mya mbili zenyi kulinganishwa na pesa za msimamo ikiwa ujehuri huwo ulitendewa mtoto mwenye umri wa cini ya myaka kumi.

**Kipengele ca 174 :**

Ikiwa kosa lenye kutajwa kwa kipengele ca 172 hapo juu kilitendeka na baba, mama ama mchungaji kulingana na kipengele ca 319 ca kitabu ca sheriya ya jamaa, mutuhumiwa, sheriya itamunyanganya mamulaka yote anayo zidi ya yule muhanga

## Sura ya 2 : Kuhusu watu ambao kukamata watoto kuwafundisha ukahaba na kuwageuza bucuruzi

**Kipengele ca 174 b :**

Ataazibiwa kwa kufungwa jela miezi mitatu hadi myaka mitano na kulipa franka hamsini elfu hadi mya moja elfu za congo zenyi kulinganishwa na pesa za msimamo :

1) Mtu yeyote ambaye kwa kumaliza haja za mwengine, atafanya ufisadi kwa kufanya usharati ama ukahaba, hata kwa hiyari ya mtu ambaye ana myaka zaidi ya kumi na minane; Umri utafaamika kiisha uchunguzi wa muganga kukiwa ukosefu wa vitabu vya kiserkali vya raia.

2) Mtu yeyote ambaye ana nyumba ambamo kufanyika usharati ama ukahaba.

3) **Msaidizi** : huyu ni mtu ambaye anaishi maisha yake yote ama nusu, kwa kutegemeya mtu ambaye anatuma kwa ukahaba.

4) Mtu yeyote ambaye anazoeya kula faida ya usharati ama ukahaba wa mtu mwengine;

**Ataazibiwa kwa azabu ambayo ipatikanayo kwa kistari ca mbele:**

1) Mtu yeyote ambaye ataonesha hazarani kitabu ama filamu ya ngono kwa watoto wa chini ya myaka kumi na minane.
2) Mtu yeyote ambaye atapitisha kwenye television michezo ama hali zisizo faa ambazo kuharibisha mila nzuri.

Wakati muhafiriwa ni mtoto wa myaka chini ya kumi na minane, azabu itakuwa myaka mitano hadi ishirini.

**Sura ya 3: Kuhusu ukahaba kwa kinguvu**

**Kipengele ca 174 c :**
Mtu yeyote ambaye atasababisha mtu moja ama wengi kutenda kitendo ao matendo zidi ya viungo vya uzazi kwa vitisho ama kupitiya unyonge wa watu hawa kuitika bila kusita ili apate faida ama vingine, ataazibiwa kifungo toka myezi mitatu hadi myaka tano ndani ya gereza.

## Sura ya 4: Kuwa na niya ao mauzi kwa mtu ukitumiya mamulaka unayo zidi ya muhanga.

### Kipengele ca 174 d :

Mtu yeyote ambaye atakazaniya kwa hali hiyo ya mauzi kwa mwengine akimwambiya maneno ama kwa matendo kwa kumutisha, kwa kumushurtisha kupitiya mamlaka anayo juu yake ili kupata faida za ngono, ataazibiwa mwaka moja hadi myaka kumi na miwili gerezani na kulipa kwa serkali franka hamsini elfu hadi mya moja elfu za congo zenyi kulinganishwa na pesa za msimamo ama moja kati ya azabu hizo. Atafuatiliwa na mahakama kulingana na kuchongewa kwake na muhafiriwa.

## Sura ya 5 : Kuhusu utumwa wa ngono

### Kipengele ca 174 e :

Atapewa azabu ya myaka tano hadi ishirini gerezani ,na kulipa kwa serkali elfu mya mbili franka za congo zenyi kulinganishwa na pesa za msimamo, mtu yeyote ambaye atashikiliwa kumunyima mtu uhuru wake kwa kununua, kuuza, kukopa ,kubadili mtu huyu kwa shabaa za ngono na kumushurtisha kufanya ngono.

**Sura ya 6; Kuhusu kufunga ndowa kwa nguvu.**

**Kipengele ca 174 f :**

Bila kuvunja mipangiliyo ya kipengele ca 336 ca sheriya ya jamaa ataazibiwa kifungo ca mwaka mmoja hadi myaka kumi na miwili gerzani na kulipa kwa serkali franka zaidi ya mya moja elfu franka za congo zenyi kulinganishwa na pesa za msimamo, mtu yeyote ambaye ana mamlaka ya uzazi ama uchunguzi juu ya mwengine, mtoto ama mukubwa, amemutoa kwa kufunga ndoa, ama kwa shabaa ya ndoa ama kumushurtisha kufanya ndoa.

Azabu ambayo kuandikwa kwa kistari ca kwanza itaongezwa mara pili ikiwa ni mtu mwenye myaka chini ya kumi na minane.

**Sura ya 7: Kuhusu kuondowa viungo fulani vya uzazi**

**Kipengele ca 174 g :**

Ataazibiwa kifungo ca myaka miwili hadi mitano nakulipa kwa serkali franka elfu mya mbili za congo zenyi kulinganishwa na pesa za msimamo, mtu ambaye kufanya kitendo ca kuharibu ama kuzuwiya viungo vya uzazi vya mtu mwengine kwa kufanya kazi vilivyo.

Ikiwa kuongowa viungo fulani husababisha kifo, azabu itakuwa kifungo cha maisha jela

**Sura ya 8: Kuhusu kufanya tendo la ndoa na mnyama**

**Kipengele ca 174 h :**

Ataazibiwa kifungo ca myaka mitano hadi kumi gerzani nakulipa franka mya mbili elfu za congo zenyi kulinganishwa na pesa za msimamo, mtu ambaye: kwaujanja,vitisho,ujehuri ama vingine vitendo vya namma hiyo akimushurtisha kufanya kitendo ca ndoa na mnyama.

Mtu ambaye kwa hiyari yake, atafanya tendo la ndoa na mnyama ataazibiwa kifungo kinaco andikwa kwa mstari wa kwanza wakipengele hiki.

**Sura ya 9 : Kuhusu kuambukiza mwengine kwa hiyari magonjwa yenye kupatikana kwa njiya ya usharati ambayo haina matibabu .**

**Kipengele ca 174 i :**

Ataazibiwa kifungo ca maisha gerezani nakulipa franka elfu mya mbili za congo zenyi kulinganishwa na pesa za msimamo, mtu ambaye kwa hiyari yake atamuambukiza mwengine magonjwa ya ngono ambayo hukosa dawa.

**Sura ya 10 : Kuuzisha na kutumikisha watoto kwa mambo ya ngono**

**Kipengele ca 174 j :**
Kila tendo lenye dalili za utumiyaji watoto ama mtu ye yote kwa shabaha za ngono kwa malipo ama kwa faida ingine, ina azibiwa kwa myaka kumi hadi ishirini gerezani.

**Sura ya 11 : Kuhusu mimba ya kinguvu**

**Kipengele ca 174 k :**
Ataazibiwa myaka kumi hadi makumi mbili gerezani, mtu yeyote ambaye ata munyima mke moja ama wanawake wengi, uhuru wao na kũ wabebesha mimba kwa kinguvu ama kwa ujanja.

**Sura ya 12 :Kufunga uzazi wa mtu kwa kinguvu**

**Kipengele ca 174 l :**
Ataazibiwa kifungo ca myaka mitano hadi kumi na mitano ndani ya jela, mtu yeyote atakae tenda kitendo juu ya mwengine kinacho mufanya kuwa tasa kama si kwa ombi ya mganga ambayo inapashwa kufasiriwa ama kwa hiyari ya muhanga mwenyewe.

**Sura ya 13 : Kuhusu maonesho ya ngono ya kuwekwa hazarani kwa watoto.**

**Kipengele ca 174 m :**
Ataazibiwa myaka mitano hadi kumi gerezani na kulipa franka kwa serkali mya moja hamsini elfu za congo zenyi kulinganishwa na pesa za msimamo mtu ye yote atakayeonesha, haizuru namna gani, mtoto akifanya kitendo ca ndoa kwa ukweli ama kufananisha, ama kuonesha viungo vya uzazi vya mtoto kwa shabaa za ngono.

**Sura ya 14 : Kuhusu ukahaba wa watoto**

**Kipengele ca 174 n :**
Ataazibiwa kifungo ca myaka tano hadi ishirini jela na kulipa franka kwa serkali mya mbili elfu za congo zenyi kulinganishwa na pesa za msimamo, mtu yeyote atakaye tumiya mtoto wa chini ya myaka kumi na minane kwa shuguli za ngono kwa kulipwa ama kwa faida yo yote ile.

Ikiwa kosa hiyo ilifanyika na mtu ambaye ana mamulaka kama muzazi ama mulishi, mutuhumiwa ataazibiwa ama kuhukumiwa na kipengele ca 319 ca sheriya ya jamaa.

**Kipengele ca ine :** Mupango wo wote wa hapo mbeleni ambao ni kinyume na sheriya hii unapigwa marufuku

**Kipengele ca tano :** Sheriya hii imeanza heshimika ama kusalimika tariki ya kutangazwa kwake.

**Imefanyika pa Kinshasa, tariki 20 july mwaka wa 2006.**

**JOSEPH KABILA.**

Imetafsiriwa naye Kemal MUSTAFA, mupasha habari kunako Redio Kivu 1, Goma/Nord-Kivu pamoja naye Jean de Dieu CIKONZA MAROYI, mupasha habari kunako Redio IRIBA FM/Bukavu/Sud-Kivu.

Kitabu hiyi ili chapwa na Maison Artistique MAM'S BUKAVU
Adresses : Simu : + 243 997714744
Email : mamsbkv@yahoo.fr

Edition 2009

Kitabu hiki cenyi kuhusika na usambazaji wa sheria nambari 06/018/ ya tarehe ishirini july mwaka wa elfu mbili na sita kwa mageuzi na nyongezo kwenyi kusudio ya sheriya ya tarehe makumi tatu january mwaka wa elfu moja mya kenda (tisa) makumi ine zidi ya buku ya hukumu katika jemuhuri ya kidem-ockasya ya Congo .

Inahusisha kwa ngambo moja wale wote wanao ujuzi mwingi katika mambo ya haki na kwa ngambo ingine wale wanao kuwa wacungaji kijamii na wengine wanao mbinu zingine kama vile combo ca kazi ili wapate kuelewa mambo mapya yaliyo wekwa ndani ya buku ya hukumu ya jamuhuri ya kidemokrasiya ya Congo na kwa kurahisisha utumizi kamilifu wa sheriya hiyo. Mungano ya wanawake zidi ya ukingo wa haki na amani « R.F.D.P.» maarufu, ilianika kitabu hiki kwa msaada kipesa wa cordaid katika muradi wake « wakusinikiza kisheriya ma binti na akinamama wahanga wa ujehuri kupitiya viungo vya uzazi katika tarafa za Walungu, Kabare na mji wa Bukavu ndani ya jimbo la Kivu ya kusini » ili kuboresha ucukuzi wa mzigo ule kisheriya ya wahanga wa ujehuri kupitiya viungo vya uzazi.

Venantie BISIMWA
R.F.D.P.